TANGAZO LA SERIKALI Na. 25 la Tarehe 17/1/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89)*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA AFYA, USAFI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 30 la 2024

**1.** Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ya Mwaka 2024 ambayo katika Kanuni Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya aya ya 3

**2.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 3 kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya msamiati "taka ngumu" kama ifuatavyo:

""taka ngumu" maana yake ni vitu visivyo vya majimaji vitokanavyo na shughuli za majumbani, mitaani, biashara, viwandani na kilimo na inajumuisha takataka au taka za vyakula, vitu visivyokuwa vya majimaji vitokanavyo na shughuli za ujenzi na ubomoaji, ufyekaji bustani na shughuli za madini, mizoga na mabaki ya magari mabovu;".

Marekebisho ya aya ya 5

**3.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 5(1) kwa kufuta na kuandika upya aya (e) kama ifuatavyo:

"(e) anakuwa na choo kilicho bora chenye maji, sakafu inayosafishika, banda imara la kudumu lililoezekwa na lenye mlango imara, bomba la kutolea hewa chafu na

lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, lililojengwa kwa vifaa vya kudumu na kisafi wakati wote;".

Marekebisho ya aya ya 7

**4.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta aya ya 7.

Marekebisho ya aya ya 13

**5.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya aya ya 13 kama ifuatavyo:

"Utengenezaji na uuzaji wa vyakula

**13.** Mfanyabiashara yeyote wa chakula hataruhusiwa kutengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote au kwenye nyumba yoyote isipokuwa kama ametimiza masharti na kanuni za afya.".

Marekebisho ya aya ya 14

**6.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya aya ya 14 kama ifuatavyo:

"Uuzaji wa vyakula vilivyopikwa

**14.** Mtu yeyote anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa atakuwa na wajibu wa kuhakikisha vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku safi lililowekwa kioo kuzuia inzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.".

Marekebisho ya aya ya 32

**7.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 32(1) kwa-

(a) kuongeza neno "au" mara baada ya alama ya nukta mkato iliyopo mwishoni mwa aya (d);
(b) kufuta alama ya nukta mkato na neno "au" mwishoni mwa aya (e) na badala yake kuweka alama ya nukta; na
(c) kufuta aya (f).

Marekebisho ya mpangilio wa namba

**8.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kubadili mpangilio wa namba za aya za 8 hadi 46 kuwa aya za 7 hadi 45, mtawalia.

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri Wa Nchi- OR-TAMISEMI*